


SHUTTERSTOCK / Enterlinedesign

# Uelewa wa sheria kuhusu vyanzo vya uandishi wa habari nchini Tanzania

Julai 2025

TrustLaw | Thomson Reuters Foundation

LawCITE Group
Property | Corporate | Litigation

Watch Africa




# Utangulizi

Mwongozo huu unalenga kuwapa waandishi wa habari uelewa kwa vitendo kuhusu mifumo ya kisheria inayohusu vyanzo vya habari nchini Tanzania. Uelewa huu utawawezesha waandishi wa habari kufahamu haki na wajibu wao wa kisheria na kuendelea kuripoti masuala yenye maslahi makubwa kwa umma. Mwongozo huu unachambua utambuzi wa vyanzo vya habari katika sheria, ulinzi wa vyanzo hivyo pamoja na masharti yanayohusu upekuzi na ukamataji wa vifaa na taarifa za waandishi wa habari.

# 1. Nini kinatafsiriwa kama chanzo cha uandishi wa habari?

Hakuna tafsiri mahsusi ya kisheria kuhusu chanzo cha habari za kiuandishi nchini Tanzania. Hata hivyo, tafsiri hiyo inaweza kupatikana kwa kuzingatia baadhi ya sheria (kwa mfano, Sheria ya Ulinzi kwa Watoa Taarifa na Mashahidi ya Mwaka 2022) ambapo chanzo cha habari kinaweza kuwa mtu binafsi au taasisi yoyote inayotoa taarifa kwa mwandishi wa habari. Vyanzo pia vinaweza kuwa nyaraka zinazobeba taarifa muhimu kwa kazi ya uandishi wa habari.

# 2. Ni sheria gani inalinda vyanzo vya uandishi wa habari?

Hakuna sheria mahsusi inayolinda vyanzo vya uandishi wa habari. Sheria mbalimbali zinashughulikia vipengele tofauti vinavyohusu vyanzo hivyo. Ingawa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitaji moja kwa moja uhuru wa vyombo vya habari, inatoa haki ya faragha[1] na uhuru wa kujieleza[2]. Hata hivyo, haki hizi si haki kamili. Katiba inairuhusu serikali kuweka masharti yanayobainisha mazingira ambayo yanaweza kuruhusu kuingiliwa kwa faragha ya mtu, kuingia nyumbani kwake, au kuchukua mali yake, pamoja na mipaka ya hatua hizo.[3] Sheria nyingine ni pamoja na:

Sheria ya Huduma za Habari, 2016: Inatoa haki ya uhuru wa vyombo vya habari na waandishi waliotambulika rasmi pamoja na vyombo vya habari vilivyosajiliwa. Pia inatoa uhuru wa kukusanya taarifa kutoka vyanzo mbalimbali.[4]

Kanuni za (Marekebisho) Huduma za Habari, 2024: Zinaweka wajibu wa kimaadili kwa waandishi wa habari kulinda vyanzo vya taarifa za siri, isipokuwa pale wanapolazimika kisheria kuvifichua.[5]

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, 2022: Inatoa ulinzi kwa taarifa binafsi na kuweka misingi na masharti ya ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa taarifa hizo.

Kanuni za Maadili ya Wanahabari: Zinaweka wajibu wa mwandishi wa habari kulinda usiri wa vyanzo vyake vya habari na kutoa taarifa hizo tu kwa amri ya mahakama yenye mamlaka.

1 Ibara ya 16 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
2 Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
3 Ibara ya 16 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
4 Kifungu cha 7 cha Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016
5 Kanuni namba 14 ya Huduma za Habari (Marekebisho) ya mwaka 2024

## 3. Je, sheria inanilinda nisifichue vyanzo vyangu vya habari? Ni katika mazingira gani naweza kulazimika kufichua chanzo cha habari?

Kama ilivyoelezwa hapo juu, waandishi wa habari wana wajibu wa kimaadili wa kulinda usiri wa vyanzo vya habari isipokuwa pale wanapohitajika na mamlaka halali kufichua vyanzo hivyo. Ni wajibu wa kimaadili kwa mwandishi wa habari kulinda vyanzo vyake vya taarifa, na kuvifichua tu endapo ameagizwa na mahakama yenye mamlaka kisheria kufanya hivyo. Mwandishi wa habari anaweza kulazimika kufichua chanzo cha habari endapo chanzo hicho kinahusishwa na shughuli ya uhalifu au uchunguzi wa jinai.

## 4. Je, chanzo cha habari kina haki gani?

Vyanzo vya habari havina ulinzi maalum wa kisheria nchini Tanzania. Katiba inatoa haki ya uhuru wa kujieleza na faragha kwa kila mtu. Katiba inampa kila mtu haki ya kutafuta, kupokea na kusambaza taarifa bila kujali mipaka ya kitaifa; na uhuru wa kuwasiliana bila kuingiliwa.



REUTERS/Emmanuel Herman

## 5. Ni mambo gani mwandishi wa habari anapaswa kuwa makini nayo anaposhughulika na chanzo cha habari?

Hakuna sheria mahsusi nchini Tanzania zinazosimamia uhusiano kati ya mwandishi wa habari na chanzo chake cha habari. Ingawa, *Kanuni za Maadili ya Wanahabari* zimeweka masharti kadhaa ambayo waandishi wa habari wanapaswa kuzingatia wanaposhirikiana na vyanzo vya habari kama ifuatavyo:

**(a)** Waandishi wa habari wana wajibu wa kimaadili kulinda usiri wa vyanzo vya habari, isipokuwa pale wanapotakiwa na mamlaka halali kufichua taarifa hizo.

**(b)** Mwandishi wa habari haruhusiwi kurekodi au kupiga picha chanzo bila ridhaa yake, isipokuwa pale ambapo rekodi au picha hiyo ina umuhimu wa kumlinda mwandishi kisheria au sababu nyingine ya msingi. Waandishi wanapaswa kupunguza madhara kwa vyanzo vyao. Hawapaswi kuchapisha taarifa zinazoweza kuhatarisha usalama wa chanzo. Wanaweza kuchapisha taarifa hizo ikiwa tu jitihada za ziada zimefanywa kuhakikisha chanzo kinaelewa madhara na kimepewa taarifa kuhusu habari hizo na baada ya kuchukua hatua za kupunguza hatari hizo.

**(c)** Waandishi wanapaswa kuepuka kutumia vyanzo vya habari visivyojulikana isipokuwa pale ambapo hakuna njia nyingine ya kupata habari husika. Wanapaswa kuthibitisha ukweli wa taarifa kutoka kwa vyanzo hivyo. Taarifa zinazokiuka siri hazipaswi kuchapishwa au kurushwa hewani, isipokuwa pale ambapo maslahi ya umma yanahitaji hivyo.

**(d)** Waandishi hawapaswi kufanya mahojiano, kupiga picha au kumtambulisha mtoto bila ridhaa ya mlezi wa kisheria au mtu mzima mwenye mamlaka ya uangalizi.

**(e)** Waandishi hawaruhusiwi kutoa pesa au zawadi ili kuvutia vyanzo vya habari kuwapa taarifa.

Kando na wajibu wa kitaaluma, kuna mambo mengine ya kisheria ambayo waandishi wanapaswa kuzingatia wanaposhughulika na vyanzo vya habari. Kuwasilisha au kusambaza taarifa za siri kwa watu wasioidhinishwa kama waandishi wa habari ni kosa.[6] Pia, waandishi wanapaswa kuhakikisha kama chanzo kinachoelekea kutoa taarifa kimesaini makubaliano ya kutofichua taarifa (*Non-Disclosure Agreement – NDA*). Ikiwa chanzo kimetia saini makubaliano ya kutofichua taarifa, waandishi wa habari wanapaswa kutambua kuwa chanzo cha taarifa kinaweza kuwa hakiruhusiwi kisheria kutoa baadhi ya taarifa husika. Kikifanya hivyo, kitakuwa kimekiuka mkataba wake na kinaweza kushitakiwa. Katika hali kama hiyo, mwandishi anaweza kutafuta chanzo mbadala kisichozuiliwa na mkataba huo lakini kinachoweza kutoa taarifa zinazofanana.

6 Kifungu cha 5 cha Sheria ya Usalama wa Taifa ya mwaka 1970




REUTERS/Francis Kokoroko

## 6. Je, naweza kuchukuliwa hatua za kisheria kwa kuhusiana na chanzo cha habari? Ni katika mazingira yapi?

Waandishi wa habari wanaweza kuchukuliwa hatua za kisheria kutokana na uhusiano wao na vyanzo vya habari ikiwa watakiuka faragha ya chanzo kama inavyolindwa na Katiba, isipokuwa kama chanzo kilitoa ridhaa ya kuchapisha taarifa za faragha. Waandishi pia wanaweza kuchukuliwa hatua za kisheria endapo watafichua taarifa binafsi za chanzo bila idhini. Aidha, waandishi wanaweza kukiuka maadili ya kitaaluma endapo hawatafuata masharti yaliyotajwa kwenye kipengele cha 5 hapo juu.

## 7. Ni katika matukio gani ninaweza kurekodi chanzo cha habari?

Kwa ujumla, waandishi wa habari wanaruhusiwa kurekodi chanzo cha habari kwa idhini yake tu, isipokuwa pale ambapo rekodi hiyo ihitajika kwa ajili ya kumlinda mwandishi katika mchakato wa kisheria au sababu nyingine ya msingi.[7] Waandishi pia wanafungwa na maadili ya uaminifu na uadilifu wa kitaaluma. Mwandishi wa habari anaweza kutumia mbinu za siri au za hila ili kuingia katika maeneo yaliyopigwa marufuku au kupata taarifa, lakini tu kwa maslahi ya umma na kwa idhini ya mhariri wake.[8] Ni kosa la jinai kunasa mawasiliano (kama vile simu) bila idhini ya kisheria.[9]

7 Kanuni za Maadili kwa Wanataaluma wa Vyombo vya Habari
8 Kanuni za Maadili kwa Wanataaluma wa Vyombo vya Habari
9 Tazama Kifungu cha 120 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroni na Posta ya Mwaka 2010

## 8. Je, jeshi la polisi linaweza kukamata nyaraka/vifaa vyangu kwa ajili ya uchunguzi? Ni katika matukio yapi wanaweza kufanya hivyo?

Ndiyo, polisi wanaweza kufanya upekuzi na kukamata nyaraka au vitu vyovyote vinavyomilikiwa na mtu yeyote, wakiwemo waandishi wa habari. Polisi wanaweza kumpekua mtu wanapomkamata na wanapaswa kuweka salama vitu vyote watakavyokuta kwa mtu huyo.[10]

Upekuzi usiohusiana moja kwa moja na kukamatwa unahitaji kibali cha upekuzi (*search warrant*) au idhini ya kufanya upekuzi. Ofisa wa polisi mwenye mamlaka katika kituo cha polisi anaweza kufanya upekuzi au kumpa polisi mwingine chini yake mamlaka ya maandishi ya kufanya upekuzi, endapo kuna sababu ya msingi ya kushuku kuwa:

**(a)** kosa limefanyika;

**(b)** kuna kitu ambacho ni ushahidi wa kutendeka kwa kosa la jinai;

**(c)** kuna kitu kitakachotumika katika kutenda kosa la jinai.[11]

Ofisa anayefanya upekuzi anapaswa kutoa risiti kuthibitisha vitu vilivyokamatwa wakati wa upekuzi.

Polisi wanaweza pia kufanya upekuzi na kukamata nyaraka za mwandishi wa habari baada ya kupata kibali cha upekuzi na ukamataji kutoka kwa mahakama.[12] Hata hivyo, polisi hawahitaji kibali cha upekuzi endapo kuna hali ya dharura.[13] Ofisa mkuu wa kituo cha polisi anaweza kuidhinisha upekuzi na ukamataji wa vifaa vya kielektroni (kama vile kompyuta, simu au vifaa vya kuhifadhi taarifa) ikiwa kuna sababu za msingi za kushuku kuwa vifaa hivyo vinaweza kuwa ushahidi wa kosa au vilipatikana kutokana na kutenda kosa.[14] Kuhusu vyombo vya habari, ofisa wa polisi mwenye sababu za msingi za kuamini kuwa chombo cha habari kimeanzishwa, kimewekwa au kinaendeshwa kinyume na Sheria ya Huduma za Habari anaweza kufanya upekuzi na kukamata vifaa vilivyopo ndani ya chombo hicho.[15] Katika upekuzi huo, polisi hawaruhusiwi kukamata au kuzuia matumizi ya vifaa vya uchapishaji, uzalishaji au usambazaji wa habari, isipokuwa pale ambapo kuna imani kuwa matumizi ya vifaa hivyo yatazuia au kuathiri uchunguzi wa kosa linalofanyika.[16]

10 Kifungu cha 24 cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 1985
11 Kifungu cha 38 cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 1985
12 Kifungu cha 41 cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 1985
13 Kifungu cha 42 cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya Mwaka 1985
14 Kifungu cha 31 cha Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ya mwaka 2015
15 Kifungu cha 60 cha Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016
16 Kifungu cha 60 cha Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016

## 9. Je, polisi wanaweza kukamata nyaraka zangu mtandaoni? Je, polisi wanaweza kunasa mawasiliano baina yangu na vyanzo vya habari, hata katika majukwaa salama/yaliyosimamiwa kwa siri?

Ndiyo, polisi wanaweza kuomba amri ya mahakama ya kunasa mawasiliano (*interception order*) kwa lengo la kupata ushahidi wa makosa yanayohusiana na ugaidi.[17] Amri hii ya kunasa mawasiliano inaweza kuruhusu:

**(a)** ufuatiliaji wa mawasiliano kupitia watoa huduma wa mawasiliano, au

**(b)** kuwekwa kwa vifaa vya kunasia mawasiliano (bugs) katika majengo kwa ajili ya kufuatilia mazungumzo au mawasiliano ya wahusika.

17 Kifungu cha 31 cha Sheria ya Kuzuia Ugaidi ya Mwaka 2002

## Kuhusu Thomson Reuters Foundation

Thomson Reuters Foundation ni taasisi iliyoasisiwa na Thomson Reuters, mojawapo ya kampuni zinazoongoza duniani katika masuala ya maudhui na teknolojia. Lengo letu ni kuendeleza jamii huru, yenye haki, na kuwa jamii yenye taarifa sahihi kuhusu nguvu ya matumizi ya vyombo vya habari, sheria na ujuzi wa data. Tunafanya kazi kuimarisha vyombo huru vya habari, kuongeza upatikanaji wa sheria na kukuza utawala bora wa biashara, jambo ambalo ni sehemu muhimu za jamii huru, zenye haki ya kupata taarifa.

TrustLaw, mradi wa Thomson Reuters Foundation, ni mtandao mkubwa zaidi duniani wa msaada wa kisheria wa bure (pro bono). Kwa kushirikiana na kampuni zinazoongoza kisheria pamoja na timu za kisheria za makampuni, TrustLaw hutoa msaada wa kisheria, tafiti zenye athari kisheria na nyenzo kwa mashirika yasiyo ya kiserikali na biashara za kijamii kwa zaidi ya nchi 190. Kupitia kuendeleza utamaduni wa huduma za kisheria za bure, TrustLaw inalenga kuongeza upatikanaji wa sheria ili kuimarisha jamii ya kiraia na kuleta mabadiliko chanya.

## Kuhusu iWatch Africa


iWatch Africa ni shirika lisilo la kiserikali la vyombo vya habari na masuala ya sera lenye hadhi na ushawishi mkubwa kitaifa. Shirika hili limejijengea nafasi muhimu katika mazingira ya sera na uandishi wa habari nchini Ghana kwa kutoa tathmini huru, ya ukweli na inayotegemea ushahidi kuhusu masuala mbalimbali.

iWatch Africa hufuatilia haki za kidijitali barani Afrika, uhalifu uliopangwa unaovuka mipaka, ukiukwaji wa haki za binadamu, mabadiliko ya tabianchi, uhifadhi wa bahari na utendaji wa serikali kwa ujumla nchini Ghana.

Kupitia matumizi ya uandishi wa habari wa takwimu, simulizi na utetezi wa sera, iWatch Africa inaunda mjadala wa kitaifa na kikanda ili kuimarisha uwazi, uwajibikaji na ushiriki wa wananchi katika utawala barani Afrika.

## Shukrani na Kanusho

Thomson Reuters Foundation na iWatch Africa wanapenda kutoa shukrani kwa timu ya kisheria ya LawCITE Group, waliotumia muda na utaalamu wao bila malipo (pro bono) kufanikisha uandaaji wa Mwongozo huu. Mwongozo huu umetolewa kwa madhumuni ya taarifa pekee. Haukusudii kuwa ushauri wa kisheria. Wasomaji wanahimizwa kutafuta ushauri kutoka kwa wanasheria waliofuzu kulingana na hali zao binafsi. Licha ya jitihada za kuhakikisha usahihi na uhalali wa taarifa zilizomo wakati wa kuchapishwa, hatuhakikishi ukamilifu wake, hasa ikizingatiwa kuwa hali zinaweza kubadilika baada ya kuchapishwa. LawCITE Group na Thomson Reuters Foundation hawatakuwa dhima au wajibu wowote kwa hatua zilizochukuliwa au kutokuchukuliwa wala kwa hasara yoyote inayotokana na kutegemea Mwongozo huu au makosa yaliyomo ndani yake.



SHUTTERSTOCK / Enterlinedesign

TrustLaw, mradi wa Thomson Reuters Foundation, ni mtandao mkubwa zaidi duniani wa msaada wa kisheria wa bure. Kwa kufanya kazi na makumpuni yanayoongoza ya sheria na timu za kisheria za mashirika, tunatoa msaada wa kisheria, tafiti za kisheria zenye matokeo makubwa na nyenzo kwa mashirika yasiyo ya kiserikali, vyombo huru vya habari na biashara za kijamii katika nchi zaidi ya 190.

Kwa maelezo zaidi, tembelea www.trust.org.

TrustLaw | Thomson Reuters Foundation